



## Taarifa za Mzazi kuhusu Elimu ya Maisha ya Familia Gredi ya 6 - 8

"Viwango vya Virginia vya elimu ya maisha ya familia hutoa mtaala wa kina na wa mfululizo wa Chekechea hadi Gredi ya 12. Inajumuisha mafunzo yanayoambatana na umri kuhusu maisha ya familia na mahusiano ya jamii, elimu ya kujiepusha na ngono, umuhimu wa kusubiri kabla ya kujihusisha na vitendo vya ngono, maumbile ya kingono na elimu ya uzazi wa binadamu. Mafunzo yamesanifiwa hivi kwamba yanahimiza uhusikaji wa wazazi, kuchochea dhana bora za kibinagsi na kutoa mbinu za kukabiliana na shinikizo la wanarika na changamoto za maisha ya kisasa kulingana na hatua za ukuaji na uwezo wa wanafunzi." (<https://www.doe.virginia.gov/teaching-learning-assessment/instruction/family-life-education>)

Nyenko zote za mafunzo zinazotumika kwenye elimu ya maisha ya familia zimeidhinishwa na kukaguliwa na Kamati ya Ushauri wa Afya ya Shuleni ya Hampton City Schools. Wazazi na walezi wana haki ya kukagua mpango wa Elimu ya Maisha ya Familia unaotolewa na kitengo cha shule yao, ikiwa ni pamoja na nyenko zote zilizoandikwa na za ziada zinazotumika kwenye mpango huo.

### Njia za kukagua nyenko:

- Unaweza kupata muhtasari wa mada na masomo kwenye [tovuti](#) ya Elimu ya Afya na Siha, kwenye kichupo cha Elimu ya Maisha ya Familia.
- Wazazi wanaweza kuangalia nyenko za mafunzo mtandaoni kuititia **Parent Square** kwa kuingia katika akaunti na kubofya Kiungo cha Nyenko.
- Nakala halisi ya nyenko zote zilizochapishwa na maelezo ya nyenko zote za sauti na video huwekwa kwenye kituo cha maudhui cha shule au kwenye matunzio ya ofisi kuu na hutolewa kwa mzazi au mlezi yeoyote anayetaka kukagua, wakati wa saa za kazi za ofisi ya shule kabla na wakati wa mwaka wa shule kwa kuweka miadi. Ili ukague nyenko, tafadhali wasiliana na mwalimu wa afya na siha wa mtoto wako.

Wazazi wanaweza kuchagua kutojumuisha watoto wao kwenye mafunzo ya maisha ya familia. **Ikiwa hungependa mtoto wako ashiriki kwenye mafunzo ya Maisha ya Familia, tafadhali tuma barua kwa mwalimu wa mtoto wako kabla mafunzo hayajaanza (angalia tarehe ya kuanza kwa mafunzo hapo chini)**. Tafadhali weka jina kamili la mtoto wako, gredi na jina la shule kwenye barua hiyo. Kwa watoto ambao hawajumuishwi, mwalimu atapanga masomo mbadala ya kuchukua nafasi ya masomo ya Elimu ya Maisha ya Familia. Ikiwa ungependa mtoto wako apokee mafunzo ya Elimu ya Maisha ya Familia, huhitaji kuchukua hatua yoyote.

Ikiwa ungependa kukagua viwango vya mafunzo ya Elimu ya Maisha ya Familia, nakala hiyo ya viwango vya mafunzo inapatikana: [HAPA](#). Ikiwa una maswali kuhusu kipengele chochote cha Mpango wetu wa Maisha ya Familia katika Hampton City Schools, tafadhali usisite kuwasiliana na ofisi ya Elimu ya Afya na Siha.

### Mada Zinazofundishwa katika Elimu ya Maisha ya Familia kwa kila gredi.

#### Gredi ya Sita:

- FLE 6.1 Usafi Binafsi  
FLE 6.3 Kubalehe  
FLE 6.4Magonjwa ya Zinaa  
FLE 6.5 UKIMWI  
FLE 6.6 Uzazi wa Binadamu  
FLE 6.6 Manufaa ya Kusubiri Kabla ya Kujihusisha na Vitendo vya Ngono  
FLE 6.8 Kuelewa Unyanyasaji wa Watoto na Kutelekezwa  
FLE 6.8 Kuzuia Unyanyasaji wa Kingono  
FLE 6.11 Kuzuia Unyanyasaji wa Kingono  
FLE 6.12 Sheria kuhusu Ulanguzi wa Binadamu

#### Gredi ya Saba:

- FLE 7.2 Anatomia na Kubalehe  
FLE 7.5 Ujumbe wa Midia na Usalama kwenye Intaneti  
FLE 7.6 Matatizo Yanayohusiana na Intaneti; ulanguzi  
FLE 7.7 Athari za Shughuli za Ngono kwa Vijana  
FLE 7.7 Manufaa ya Kusubiri Kabla ya Kujihusisha na Vitendo vya Ngono  
FLE 7.8 Ishara na Dalili za Ujauzito  
FLE 7.10 Kuzuia Dhuluma za Kingono  
FLE 7.11 Magonjwa ya Zinaa

#### Gredi ya Nane:

- FLE 8.1 Hatua za Ukuaji wa Binadamu  
FLE 8.1 Mapitio ya Anatomia  
FLE 8.3 Kulinda Taarifa Binafsi Mtandaoni  
FLE 8.5 Kuchumbiana/Unyanyasaji kwenye Mahusiano ya Kuchumbiana  
FLE 8.7 Elimu ya Kujiepusha na Ngono  
FLE 8.11 Kuzuia Magonjwa ya Zinaa  
FLE 8.11 Kuzuia Ujauzito  
FLE 8.13 Kuzuia Dhuluma za Kingono  
FLE 8.14 UKIMWI  
FLE 8.10 Matatizo Yanayohusiana na Ujauzito kwa Vijana

### Mafunzo ya Maisha ya Familia yatafanyika \_\_\_\_\_.